**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAWASILIANO ARDHI NA NISHATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

*Mheshimiwa Spika,*

Kama ilivyo ada naomba uniruhusu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na huruma ambaye ametuwezesha kukutana hapa tukiwa na afya njema, amani na utulivu na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu yanayochangia katika kujenga ustawi wa nchi yetu.

*Mheshimiwa Spika,*

Pia, tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana katika kikao chetu cha leo kwa ajili ya kupokea utekelezaji wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi pamoja na kutafakari mipango ijayo katika kuyafikia malengo ya taifa letu.

*Mheshimiwa Spika,*

Napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutokana na juhudi zake kubwa za kuwaletea maendeleo wananchi wake. Naomba tuendelee kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia afya thabiti, hekima, busara na ustahimilivu katika kuiongoza

nchi yetu.

*Mheshimiwa Spika,*

Vile vile, napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii mbele ya Baraza lako tukufu kuweza kuwasilisha maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na muelekeo wa bajeti ya mwaka wa fedha wa 2023/2024.

*Mheshimiwa Spika,*

Nitumie pia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa utendaji wao mzuri wa kazi zao na ushirikiano mkubwa wanaoipatia Kamati hii katika kutekeleza majukumu yake ya kuisimamia Wizara hii.

*Mheshimiwa Spika,*

Vile vile, pongezi za dhati kabisa ziende kwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati yangu kwa kazi nzuri wanayoifanya na ushirikiano wanaouonesha kwa pamoja katika kutekeleza majukumu ya kazi zetu kwa muda wote, naomba sasa niwatambue wajumbe hawa kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Yahya Rashid Abdulla | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Hussien Ibrahim Makungu | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Bahati Khamis Kombo | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Kombo Mwinyi Shekhe | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Rahma Kombo Mgeni | Katibu |
| **8.** | Ndg. Himid Haji Choko | Katibu |

*Mheshimiwa Spika,*

Tukianza kuchambua utekelezaji wa Wizara hii tunayoijadili leo tunabaini kwamba hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Machi, 2023, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imekusanya **Tsh. Bilioni 2.6** sawa na **106%** ya makadirio ya miezi tisa.

*Mheshimiwa Spika,*

Kamati inaipongeza Wizara kwa kuvuka malengo ya ukusanyaji na ni matumaini yetu kwamba juhudi zaidi zitachukuliwa ili kupiga hatua zaidi kwa robo ya mwisho iliyobakia.

*Mheshimiwa Spika,*

Kupitia *Programu Kuu ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti,* Kamati imejengwa na matumaini makubwa baada ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuendeleza na vikao vya majadiliano na Kampuni mbali mbali zilizoonesha nia ya kuwekeza katika miradi ya nyumba za makaazi za bei nafuu kwa wananchi.

*Mheshimiwa Spika,*

Tunaamini kwamba iwapo uwekezaji huu utafanikiwa utapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la makaazi kwa wananchi wetu.

*Mheshimiwa Spika,*

Vile vile, Kamati inasisitiza haja ya kuongeza kasi katika shughuli za mapitio ya Sera na Sheria zinazosimamia sekta ya ardhi ili ziweze kutumika na kukidhi haja ya matumizi kwa wakati tulionao.

*Mheshimiwa Spika,*

Kamati yangu inaomba kukamilishwa kwa shughuli hizo kwani muda mrefu sasa umepita na shughuli hiyo haijakamilika.

*Mheshimiwa Spika,*

Kamati yangu bado inahuzunishwa na suala la migogoro ya ardhi inayoendelea kuibuka kila siku. Mheshimiwa Spika, tukisoma **Kiambatanisho F2** katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri tutagundua kwamba jumla ya mashauri mapya **165** yamefunguliwa kwa kipindi hiki Unguja na Pemba. Takwimu hizi ni kubwa na zinathibitisha kuendelea kwa kasi tatizo la migogoro ya ardhi katika jamii.

*Mheshimiwa Spika,*

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati yangu inaitaka Wizara hii kuendelea na zoezi la utoaji wa elimu kwa wananchi ili waweze kufahamu matumizi na umiliki halali wa ardhi na hatimae kujikinga na kujiepusha na migogoro ya ardhi hapa nchini.

*Mheshimiwa Spika,*

Ili Kamisheni ya Ardhi iweze kutekeleza shughuli zake za Utawala, Ugawaji na Usimamizi wa Ardhi, Uratibu usajili wa Ardhi, Upimaji na Utoaji wa Ramani za Ardhi pamoja na Upangaji wa Miji na Matumizi ya Ardhi inahitaji kuwa na vitendea kazi pamoja na afisi za uhakika.

*Mheshimiwa Spika,*

Kwa bahati mbaya Kamisheni ya Ardhi inakabiliwa na uchakavu mkubwa wa majengo yake ya Forodhani kwa Unguja pamoja na Macho Mane - Pemba.

*Mheshimiwa Spika,*

Kamati yangu ilifanya ziara ya kukaguwa majengo hayo na kushuhudia hali mbaya ya uchakavu inayotishia usalama wa wafanyakazi na nyaraka zinazohifadhiwa katika majengo hayo.

*Mheshimiwa Spika,*

Kwa msingi huo, Kamati inaomba kuchukuliwa kwa hatua za dharura ili kuhami hali hiyo kabla ya kuleta maafa kwani kifungu cha 77 cha Sheria ya Utumishi wa Umma No. 2 ya mwaka 2011 kinaelekeza kuwa Watumishi wa umma wanatakiwa kufanya kazi katika mazingira bora na salama.

*Mheshimiwa Spika,*

Kamati yangu haikuridhishwa na kiwango cha mapato kilichokusanywa na Wakala wa Majengo kupitia *Programu ya Maendeleo ya Makaazi* kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

*Mheshimiwa Spika,*

Katika kufuatilia hilo, tumebaini kuwa miongoni mwa kianzio cha mapato cha Wakala huyu ambacho ni mashine ya kusagia kokoto ni chakavu, Hata hivyo, kwa hivi sasa mashine hiyo inasimamiwa kiuendeshaji na mwananchi wa kawaida bila ya kuwa na mkataba wowote ingawa mwananchi huyo huipatia fedha Taasisi hiyo kutokana na kiwango cha uzalishaji kinachofanyika.

*Mheshimiwa Spika,*

Kamati yangu ilishitushwa na hali hiyo na inaishauri Serikali kuiuza mashine hiyo kwa kuwa ni ya muda mrefu na imekuwa ikiharibika mara kwa mara.

*Mheshimiwa Spika,*

Sambamba na hilo, Kamati yangu inaishauri Serikali kufunga mikataba na wale wote ambao wanatumia mali za Serikali ili kuepusha hoja zisizo na msingi.

*Mheshimiwa Spika,*

Miongoni mwa malengo makuu ya Programu ya Maendeleo ya Makaazi ni usimamizi wa shughuli za ujenzi na kuhakikisha ubora wa majengo hapa nchini chini ya usimamizi wa Wakala wa Majengo (ZBA).

*Mheshimiwa Spika,*

Licha ya jukumu hilo zito alilopewa Wakala huyu, Kamati yangu ina wasiwasi na uwezo wa kiutendaji wa Wakala wa Majengo kutokana na changamoto mbali mbali inayoikabili Taasisi hii ikiwemo, uhaba wa rasilimali watu, fedha,  vitendea kazi, ukosefu wa teknolojia za kisasa, kutokupewa nafasi ya kutekeleza ipasavyo jukumu lake la msingi la kusimamia miradi ya Serikali.

*Mheshimiwa Spika,*

Mambo yote hayo yanapelekea Wakala huyu kuonekana kuwa hatekelezi vyema shughuli zake. Mheshimiwa Spika, kutokana na dosari hizo zilizobainika, Kamati yangu inaishauri Serikali kuipa kipaumbele Wakala wa Majengo ili iweze kupatikana tija ya kuanzishwa kwa Taasisi hii.

*Mheshimiwa Spika,*

Mwanzoni mwa uwasilishaji wangu wa utekelezaji wa Wizara hii, Kamati yangu ilitoa sifa kwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kutokana na kitendo cha kuvuka lengo la ukusanyaji wa mapato kwa mwaka huu wa fedha.

*Mheshimiwa Spika,*

Hata hivyo, kulingana na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kitaasisi, inaonesha kwamba Shirika la Nyumba limefanya vibaya katika eneo hilo muhimu kwa maendeleo ya Shirika hilo, kwani katika mwaka unaomalizika lilipangiwa kukusanya **Tsh. Bilioni 9.902** ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2023 Shirika lilikusanya Tsh. **Bilioni 2.026** sawa na asilimia **20.46%** tu.

*Mheshimiwa Spika,*

Kamati yangu haikuridhika na hali hiyo na inaliomba Shirika, kuongeza bidii katika kuwashajihisha Wapangaji wake kusawazisha kodi zao.

*Mheshimiwa Spika,*

Tunaelewa kuwa miongoni mwa Wapangaji wa Shirika la Nyumba ni baadhi ya Watendaji wa Umma, kwa msingi huo, Kamati yangu inaishauri Serikali kuanzia mwaka mpya wa fedha ujao kuhakikisha kuwa inawakata moja kwa moja kwenye mishahara yao Watendaji wao waliokodi nyumba katika Shirika hili kama mikato mengine inavyofanywa, kwa mfano; Mkato wa Income Tax, ZSSF na kadhalika ili Shirika liweze kupata kodi yake kwa wakati kwa maendeleo ya Shirika hili.

*Mheshimiwa Spika,*

Pamoja na hayo, Kamati yangu inapongeza mipango ya Shirika la Nyumba ya mwaka wa fedha 2023/2024 ya kujenga nyumba za bei nafuu katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

***Mheshimiwa Spika,***

Hatua hiyo ni nzuri kwani itaondosha tatizo la nyumba za makazi kwa Watumishi wa Umma na wananchi kwa ujumla.

***Mheshimiwa Spika,***

Kamati yangu inaendelea kuikumbusha Serikali kuziimarisha kifedha sekta zinazosimamiwa na Wizara hii ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji pamoja na kuweza kukusanya mapato yatokanayo na sekta hizo kwa wingi na kwa wepesi. Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inakumbushia hilo kwa kuwa inaamini kuwa kuimarisha sekta hizo ***sio kupoteza bali ni kuwekeza*** na mafanikio yake yataonekana katika kipindi kifupi.

***Mheshimiwa Spika,***

Kwa mara nyengine tena napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha hotuba yangu kwa niaba ya Kamati na pia napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuifatilia kwa ukaribu sana hotuba yangu hii na kwa kunisikiliza. Ni matumaini yangu kuwa Wajumbe wataichangia, wataijadili na hatimae kuyapitisha makadirio ya Bajeti ya Wizara hii ili tumuwezeshe Mheshimiwa Waziri kutekeleza Shabaha walizojipangia.

***Mheshimiwa Spika,*** Naomba kuwasilisha.

Ahsante,

………….………………..

(Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir)
MAKAMO MWENYEKITI,
KAMATI YA MAWASILIANO ARDHI NA NISHATI,
BARAZA LA WAWAKILISHI,
ZANZIBAR